# CLASS 6 MID TERM 2 2020

# KISWAHILI

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU** — Saa 1 Dakika 40

1. Tumia penseli ya kawaida tu.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-
   **(i) JINA LAKO** **(ii) JINA LA SHULE YAKO**
3. Kwa kila swali onyesha kwa kupiga mstari kwenye mabano lile jibu ulilolichagua limeandikwa.

***Vifungu vifuatavyo vina nafasi zilizoachwa wazi kutoka nambari 1- 15. Chagua jibu sahihi ujaze nafasi hizo***

Hadija alikuwa akienda ____1____. Njiani alikutana na marafiki ___2___. ___3___ ya kuenda kusoma, waliamua kuanza kucheza. Walicheza kwa muda ___4___ sana. Waliposhtukia waligundua kuwa ni adhuhuri.

Ilikuwa vigumu kuenda chuoni ___5___ kurudi nyumbani. Adhabu iliwangoja kila upande. Walikuwa na wasiwasi kama ___6___. Waliingia msituni na kujificha. Kwa sababu ya ___7___, walilala ___8___. Usingizi ulikuwa ___9___ pono. Walishtuka wakati mama mmoja alipowaamsha. Alikuwa ameenda msituni kutema kuni.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | katika shuleni | kwa shule | shule | shuleni |
| 2. | zake | yake | wake | lake |
| 3. | Badala | Baada | Kabla | Bila |
| 4. | lirefu | refu | mrefu | ndefu |
| 5. | ila | wala | ili | walakini |
| 6. | mzee | mjanga | waasi | mjuha |
| 7. | uchovu | uchofu | mchovu | mchefu |
| 8. | zi | fyu | feee | fofofo |
| 9. | ya | wa | la | kwa |

Kuna haki ___10____ za watoto. Baadhi ya haki ____11____ ni kupata elimu ____12____ ni msingi wa maisha ____13____. Watoto hupata elimu kwa kuhudhuria ____14____. Aidha, kupata lishe bora na matibabu ni haki ____15____ za watoto.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | mingi | nyingi | jingi | wengi |
| 11. | hizi hizi | hizo hizi | haya haya | hii hii |
| 12. | ambao | ambaye | ambayo | ambalo |
| 13. | mbora | mabora | kibora | bora |
| 14. | hospitali | shule | soko | kanisa |
| 15. | zinginezo | nyinginezo | wenginezo | jinginezo |



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Kutoka swali la 16-30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Usemi 'fyata ulimi" una maana gani?
A. Piga mbinja B. Nyamaza
C. Kula sana D. Kuwa mgonjwa

17. Ni sentensi ipi iliyo katika jinsi ya kutendewa?
A. Waliosha chumba chao asubuhi.
B. Mwalimu alisomesha vizuri.
C. Alipikiwa chakula murua.
D. Wanarandaranda mitaani.

18. Jina jingine la 'bombo' ni;
A. kaptura B. gagro
C. chupi D. kocho

19. Ni kipi **kivumishi sifa** katika sentensi hii;
Meza ndogo imeibiwa leo.
A. meza B. ndogo
C. imeibiwa D. leo

20. Dada ya mama huitwa:-
A. mkoi B. shangazi
C. halati D. ami

21. Tumia kirejeshi 'ndi' kwa usahihi;
Minyoo hao _____ waliomharibu afya.
A. ndio B. ndizo
C. ndiyo D. ndilo

22. Kitenzi 'angaza' katika kauli ya kutendwa kitakuwa;
A. angazia B. angazwa
C. angaziwa D. angavu

23. Chagua jina la kikembe cha nguruwe.
A. jana B. kitungule
C. kivinimbi D. kiluwiluwi

24. Andika tarakimu kwa nambari
Laki tano, mia tisa sitini na tisa.
A. 50,996 B. 500,969
C. 5669 D. 50,169

25. Tumia 'o-ote' kwa usahihi.
Kiboko _______ hukaa majini.
A. yeyote B. chochote
C. wowote D. yoyote


26. "Meli" ni nomino katika ngeli ya;
A. LI - YA B. U - ZI
C. I - ZI D. U - U

27. Andika sentensi kwa wingi.
Ubavu umevunjika.
A. Bavu zimevunjika.
B. Mabavu yamevunjika.
C. Vibavu vimevunjika
D. Mbavu zimevunjika

28. Kamilisha methali hii.
Mwana wa kuku hafunzwi;
A. kula B. kuruka
C. kuwika D. kuchakura

29. Chombo cha seremala ambacho hutumiwa kushikilia mbao imara inapofanyiwa kazi huitwa:-
A. bisibisi B. jiriwa
C. timazi D. nyundo

30. Umbo hili linaitwaje?



A. Pia B. Duara dufu
C. Mche D. Duara

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40**

Hakuna mtu duniani ambaye hana marafiki. Marafiki huwa wa aina mbili. Kuna wale ambao ni wandani na wengine ni wale wanaojifanya wazuri lakini ndani ni mbwamwitu.

Macharia alikuwa na bahati ya kuwa na kazi ya kutajika. Alikuwa na ngweje nyingi. Marafiki walijaa kwa sababu kulikuwa na kitu cha kuliwa. Kila wakati gari lake lilikuwa limejaa marafiki. Walimpeleka kununua vifaa vya nyumbani. Hakujua walikuwa wakimwonea gere. Walicheka mdomoni lakini moyoni walikuwa wamenuna. Watu hawa walipata kujua siri za Macharia zote. Aliwapuuza mke na watotowe na kuwa hana muda na familia yake. Kila walipolalamika aliwakemea. Waliamua kunyamaza.



E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Bwana Macharia alipata fursa ya kuenda ng'ambo kuhudhuria mkutano kwa niaba ya kampuni. Alipanga safari yake bila siri na kuondoka. Mke na watoto waliachwa. Marafiki walipanga kumwibia Macharia. Waliwatafuta wezi na kukodisha lori. Walienda kwa Macharia na kumwambia mkewe kuwa Macharia alikuwa amekopa bidhaa zote na alikuwa amekataa kulipa.

Mkewe Macharia aliwasihi wangojee Macharia arudi kutoka ng'ambo lakini walitia masikio yao makenta. Baada ya mwezi mmoja Bwana Macharia alirudi nyumbani na kukuta familia yake ikilala sakafuni. Alikanusha kuwa hakuna siku ambayo alikopa chochote. Ulikuwa ni mpango wa wizi. Walipopiga simu kwenye nambari walizopewa, waliduwaa walipopokea ujumbe kuwa simu hiyo haifanyi kazi tena. Bwana Macharia aligundua kuwa marafiki zake walihusika lakini kwa sababu hakuwa na ushahidi, aliamua kunyamaza na kukubali kuwa walikuwa wameibiwa.

**31.** Marafiki ambao hujifanya wazuri lakini ndani ni mbwamwitu ni;
A. wale ambao hawakutakii mema.
B. wale ambao huwa tayari kukufa nawe wakati wa shida
C. wale ambao mlijuana hivi karibuni
D. marafiki wa mbali kidogo

**32.** Habari hii inatuonyesha kuwa Bwana Macharia alikuwa:-
A. fukara B. mjane
C. mkwasi D. mchoyo

**33.** Licha ya Macharia kuwa na pesa nyingi;
A. aliwapa watu wa jamaa yake kichochu
B. hakuwa na muda na familia yake
C. aliwatunza watoto na mke wake kwa kuwapa hela na muda
D. alimtaliki mke wake na kutumia pesa vibaya

**34.** Safari ya Macharia katika nchi ya kigeni sababu yake ilikuwa:-
A. kutafuta mahali pa kufanyaia biasharia
B. kuwasilisha kampuni katika mashindano
C. kutaka kuzuru kampuni katika mkutano
D. kuwasilisha kampuni katika mkutano

**35.** Udhaifu mkubwa zaidi wa Macharia ulikuwa
A. kuwa na marafiki wengi
B. kutoficha siri zake
C. kuenda nchi ya kigeni
D. kuwakimu watoto na mama yao

**36.** Mpango wa kumwibia Macharia ulikuwa;
A. umepangwa na wafanyakazi wa Macharia.
B. ni ujambazi wa kawaida ambao hakuwa aliyeupanga
C. umepangwa na wandani wake ambao walizifahamu siri zake
D. umepangwa na mke wa Macharia

**37.** Unafikiri kwa nini wezi wale walienda kuiba bila wasiwasi?
A. Walikuwa na silaha hatari.
B. Walijua alipokuwa Macharia na bidhaa ambazo alikuwa nazo nyumbani.
C. Mke wa Macharia alikuwa mwoga na hakuweza kuwazuia
D. Wao ndio waliomkopesha kila kitu

**38.** Kwa nini mke wa Macharia aliwaamini wezi wale?
A. Hakuwa amejua bidhaa zile.
B. Alikuwa akiwafahamu wezi wale kuwa ni wao waliowakopesha.
C. Alidhihirisha ujinga wake katika kufanya uamuzi.
D. Alilazimishwa kuamini hivyo.

**39.** Safari ya Macharia ilikuwa ya muda gani?
A. Mwezi mmoja B. Mwaka mmoja
C. Juma moja D. Siku chache

**40.** Taja methali inayooana na habari hii.
A. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.
B. Kikulacho ki nguoni mwako.
C. Adui mpende
D. Msafiri ni aliye pwani.


Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Tarehe 12 Disemba 1963 ni siku ambayo Wakenya, hasa wazalendo hawawezi kuisahau kabisa. Ni siku ambayo tulipyakua uhuru wetu kutoka kwa Mwingereza. Watu wa mataifa mbalimbali walikusanyika katika uwanja wa Jamhuri. Ilipowadia saa sita kasoro dakika tano za usiku, taa zote zilizimwa. Giza totoro likatanda. Saa sita za usiku bendera yetu tukufu yenye rangi nyeusi, nyeupe, nyekundu na kijani ilitwekwa na ile ya Mwingereza ikateremshwa. Ving'ora, vigelegele, vifijo, fataki, shangwe, mizinga na kila aina ya furaha vyote vilijitokeza na kuzidi kuupamba uwanja. Mkombozi wa taifa letu akaapishwa kuwa waziri mkuu wa kwanza wa nchi huru ya Kenya, kisha mawaziri wake nao wakaapishwa. Baraza hilo jipya lilikuwa la Waafrika wote isipokuwa wazungu waliokuwa wachache mno.

Wazalendo hawakutosheka kwani walikuwa wakikerwa na kuweko kwa gavana aliyekuwa akimwakilisha Malkia wa Uingereza na alikuwa na mamlaka fulani serikalini. Njia ya kumwondoa gavana huyo ilikuwa ni kulifanya taifa letu kuwa Jamhuri. Jambo hili likatekelezwa tarehe 12 Disemba 1964 na hapo Mzee Kenyatta akachukua hatamu ya kuliongoza taifa na kuwa rais wa kwanza. Umaarufu wa nchi yetu ulisambaa katika mabara yote ulimwenguni hasa kutokana na uongozi mwema wa mabalozi wetu.

Mazao yetu kama kahawa, chai na pareto yametupatia sifa. Mbuga zetu, fuo za bahari na mandhari ya nchi yetu vyote ni mnaso wa watalii.

41. Wakenya wanaikumbuka tarehe 12 Disemba 1963 kwa sababu;
    A. ni siku ya mashaka ya mkoloni
    B. ndiyo siku uhuru wa wakazi wa bara zima ulinyakuliwa.
    C. ni siku ambayo walipata kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine.
    D. ni siku ambayo giza totoro lilitanda kote

42. Ni rangi ipi kwenye bendera ni ishara ya kilimo?
    A. Nyeupe B. Nyekundu
    C. Nyeusi D. Kijani

43. Ni neno gani linalomaanisha watu ambao wanaipenda nchi yao na walio tayari kuifia?
    A. Wazalendo
    B. Waafrika kindakindaki
    C. Wakenya
    D. Wenyeji

44. Kulingana na aya ya pili, baraza jipya la mawaziri lilihusisha;
    A. waafrika pekee
    B. wazungu pekee
    C. waafrika na wazungu wachache
    D. marais pekee

45. Uhuru ni kinyume cha:-
    A. ushindi B. kufungwa
    C. mateso D. utumwa

46. Hivi vyote vilijitokeza isipokuwa:-
    A. vigelegele, vifijo na shangwe
    B. mizinga, ving'ora na fataki
    C. vigelegele na fataki pekee
    D. ving'ora vifijo na shangwe

47. Gavana alikuwa akiwakilisha nani?
    A. Wakenya
    B. Malkia wa Uingereza
    C. Wazalendo
    D. Waziri mkuu

48. ________ ndilo jina jingine la bendera.
    A. Mlingito B. Bura
    C. Beramu D. Hatamu

49. Waziri huwakilisha:-
    A. bunge B. wizara
    C. serikali D. baraza

50. Taifa la Kenya lilikuwa Jamhuri mwaka wa
    A. 1964 B. 1963
    C. 1962 D. 1960



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com